**السلام مع النفس والكون**

**AMANI KWENYE NAFSI NA ULIMWENGU.**

**Hotuba ya Kwanza.**

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, mwenye kusema katika Kitabu chake: {**Na Mwenyezi Mungu analingania kwenye nyumba ya amani na kumuongoza amtakaye kwenye njia iliyonyooka**}. Ninashuhudia kuwa hakuna Mola wa Haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake na asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume Muhammad S.A.W ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu mteremshie sala na salamu Mtume Muhammad pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba wake na wale wote waliomfuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya Utangulizi**:

Hakika amani ni yenye thamani kubwa kwa mwanadamu, dini yetu ya Kiislamu imetoa shime kubwa katika kuimarisha hiyo amani, kwani dini yetu ni dini ya amani, na Mtume wetu S.A.W ni Mtume wa amani, maamkizi yetu duniani ni neno amani, pepo ndio nyumba ya amani, na salamu za watu wa peponi wakiwa ndani ya pepo ni amani, salamu za Malaika kwa watu wa peponi ni amni, ambapo Anasema Mola Mtukufu: {**Enyi mlio amini! Ingieni katika Uislamu kwa ukamilifu, wala msifuate nyayo za Shetani hakika yeye kwenu ni adui aliye wazi**} na Anasema Mola Mtukufu: {**Hao watapata nyumba ya salama kwa Mola Mlezi wao**} na anasema Mola Mtukufu: {**Na maamkio yao humo ni amani**} na Anasema tena Mola Mtukufu: {**Na malaika wanaingia katika kila mlango * Wakiwaambia Assalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu, kwa sababu ya mlivyo subiri! Basi ni mema mno malipo ya Nyumba ya Akhera**}.

Nafasi ya amani na utukufu wake Mwenyezi Mtukufu amejiita Yeye mwenyewe kuwa ni "Amani" akasema Mola Mtukufu: {**Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipokuwa Yeye tu. Mfalme Mtakatifu, Mwenye amani, Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake, Mwenye nguvu, Anaye fanya analo litaka, Mkubwa, Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayo mshirikisha nayo**} na yalikuwa miongoni mwa maombi ya Mtume S.A.W baada ya kumaliza swala ni kusema: "*Ewe Mwenyezi Mungu Wewe ndio Mwenye*

*amani na kwako ndiko inakotoka amani umetakasika ewe Mwenye utukufu na Mwingi wa heshima*".

Hakika amani katika Uislamu ni amani kwa wote, na Muislamu wa kweli ni mwingi wa msamaha kwenye nafsi yake, ni mwenye amani ya kweli kwa watu wake na ndugu zake pamoja na jirani zake na marafiki zake pia kwa watu wote, ambapo anasema Mtume wetu S.A.W: "*Muislamu wa kweli ni mwenye kuwapa amani watu kwa ulimi wake na mikono yake*" na anasema Mtume S.A.W: "*Naapa kwa Mweneyezi Mungu, hana imani, naapa hana imani, naapa hana imani, akaulizwa: Ni nani ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema, ni yule jirani zake hawapati amani kwa dhuluma zake*", pindi alipoulizwa Mtume S.A.W kuhusu mwanamke mwenye msimamo isipokuwa tatizo lake ni huleta kero na maudhi kwa jirani zake kwa ulimi wake, ndipo Mtume S.A.W akasema: "*Hakuna ubora kwake kwani ni mwanamke wa motoni*".

Tunasisitiza kuwa hii amani haifikiwi isipokuwa kupitia nafsi zilizo safi zikiendeshwa na misingi ya Imani na utu, miongoni mwake ni kuwa mwanadamu na sura moja nje yake ni sawa na ndani yake, wala si kuwa mwenye sura mbili ambazo anakutana na hawa na sura hii na wengine kwa sura nyengine, kwani anasema Mtume S.A.W: "*Miongoni mwa watu wa shari ni wale wenye sura mbili ambazo anakuja kwa hawa na sura moja na kwa wengine na sura nyengine*".

Pia: Mwanadamu kuwa ni mwenye kupenda kheiri kwa watu wote, mpole mwenye upendo wepesi na ulaini ambapo anasema Nabii wetu S.A.W: "*Hataamini mmoja wetu mpaka apende kwa ndugu yake kile anachopenda kwenye nafsi yake*" na anatakiwa kuwa ufunguo wa mambo ya kheiri wenye kufunga milango ya shari, kwani anasema Mtume S.A.W "*Hakika miongoni mwa watu ni funguo za kheiri ni wenye kufunga shari, pia miongoni mwa watu ni fungua za shari wenye kufunga kheir, hivyo amefaulu mwenye kujaaliwa na Mwenyezi Mungu funguo za kheiri mikononi mwake, na ana adhabu kali mwenye kuwa na funguo za shari mikononi mwake*".

Miongoni pia: Kuamini kila mwanadamu ana haki kwa mwengine ya kuishi maisha bora yenye amani na utulivu, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu ameumba watu wakiwa tafauti ambapo anasema Mola Mtukufu: {**Lau angetaka Mola wako wangeamini wote waliopo ardhini, hivi wewe unatenza nguvu watu ili wawe**

**Waumini**}, na anatakiwa kuamini kuwa kuna mgawanyo wa kibinadamu wa pamoja uliokusanywa na Sharia zote za mbinguni, unaopelekea ulazima ili kueneza utulivu na amani ya nafsi na wote katika jamii.

**Hotuba ya Pili**.

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu, swala na salamu ziwe kwa Mtume wa mwisho naye ni Mtume wetu Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Muislamu anaishi katika amani na ulimwengu wote, hapaswi kufanya maudhi kwa wanyama wala kuchoma moto mimea wala kuharibu mti wala matunda, bali ni mjenzi mwenye manufaa mwenye kupenda kheiri wala sio shari, mwenye kupenda ujenzi na wala sio uharibifu, mwenye kupenda maendeleo na wala sio uharibifu wa maendeleo, wala kuleta uharibifu duniani, kwani Mtume wetu S.A.W alikuwa anajenga misingi ya hii amani ya dunia, yeye amekuwa ni rehma kwa walimwengu wote, ambapo anasema Mola Mtukufu: {**Na wala hatukukutuma isipokuwa uwe na rehema kwa walimwengu wote**} linaonekana hili wazi pale Mtume S.A.W alipoingia kwenye bustani mmoja katika watu wa Madina na akakuta ndani ya hiyo bustani kuna ngamia, yule ngamia alipomuona tu Mtume S.A.W akainama na macho yake yakiwa yanatoa machozi. Mtume S.A.W akamuendea kisha akaanza kumpangusa kichwa chake akanyamaza, ndipo Mtume S.A.W akauliza ni nani mwenye ngamia huyu? Akatokea kijana mmoja akasema: Ni wangu mimi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ndipo Mtume S.A.W akasema: "*Hivi humuogopi Mwenyezi Mungu kwenye huyu Mnyama ambaye Mwenyezi Mungu amekumilikisha kumsimamia? Kwani huyu mnyama amenishitakia kuwa wewe unamuweka na njaa pamoja na kumtesa*".

Ni uzuri ulioje mwanadamu akaishi kwa kuwa na amani kwake mwenyewe, kuwa na amani kwa ukoo wake, kuwa na amani kwa familia yake, majirani zake, wenzake, marafiki zake, kwa jamii na ulimwengu kwa ujumla.

**Tunakuomba Mwenyezi Mungu tujaaliye kuwa ni miongoni mwa watu amani, na utuingize kwa huruma yako kwenye nyumba ya amani Peponi.**